



Kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani katika hali za dharura

Kitabu cha mwongozo kwa wafanyi kazi na wajitolea wa Shirika la Msalaba Mwekundu / Hilali Nyekundu



International Federation
of Red Cross and Red Crescent Societies

Ajenda ya Ulimwengu ya Shirikisho la Kimataifa (2006 – 2010)

Kwa miaka miwili ijayo, malengo kwa jumla ya Shirikisho yatakuwa kutekeleza aula na malengo yafuatayo:

Malengo yetu

Lengo 1: Kupunguza idadi za vifo, majeraha na athari za mabaa.

Lengo 2: Kupunguza idadi za vifo, magonjwa na athari za magonjwa na dharura za afya kwa jamii.

Lengo 3: Kuimarisha uwezo wa jamii ya nchi, vyama vya uraia na Shirika la Msalaba Mwekundu kushughulikia hali za haraka zisizokuwa na salama.

Lengo 4: Kukuza staha kote na heshima za binadamu, na kupunguza uhasama, ubaguzi na kutoshirikisha kijamii.

Aula zetu

Kuboresha uwezo wetu nchini, eneo na kimataifa kuitikia hali za mabaa na dharura za afya kwa jamii.

Kuongeza shughuli zetu na uwezo wetu kuimarisha hali za afya kwa jamii zisizokuwa na salama, kuzuia magonjwa na kupunguza hatari zinazosababisha baa.

Kuimarisha zaidi programu na shughuli zetu za utetezi zinazohusu VVU (HIV) na UKIMWI.

Kuangalia upya utetezi wetu kwa aula za kibinadamu, hasa kupambana na uhasama, shutumu na ubaguzi, na kutangaza kupunguza hatari zinazosababisha baa.

@ Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

Sehemu yoyote ya kijitabu hiki haiwezi kudondolewa, kunakiliwa, kutafsiriwa kwa lugha nyingine au kuchukuliwa kutumika kitaifa Bila kupata idhini kutoka Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu, ila tu chanzo chake kimeelezwa vyema.

Katao

Kwa vile hati hii inasudiwa kuwa kitabu cha mwongozo wa kawaida za kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani, mara nyingi bidhaa fulani zinazotumika katika hali za dharura zimetajwa. Haya hayamaanishi kwamba Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu linapendekeza na kutia kidole kwa bidhaa hizi.

Picha ya mbele: Shirikisho la Kimataifa

Shukrani kubwa kwa wale wote walioweza kuchapishwa kwa mwongozo huu. Hasa Rebecca Kabura, Angelika Kessler na Daniele Lantagne.

2008

Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu
S.L.P 372
CH-1211 Geneva 19
Uswizi (Switzerland)
Simu: +41 22 730 4222
Kipepesi: +41 22 733 0395
Barua pepe: secretariat@ifrc.org
Mtandao: www.ifrc.org

> Yaliyomo

Ubora wa Maji kwa Ufupi	2
Utangulizi wa Kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani	4
Taratibu za kutibu maji ya nyumbani	6
Kupitisha kwa kichujio	6
Usafishaji	7
Kuchemsha	8
Nguvu za jua	10
Usafishaji kwa Kemikali	12
Mashapo	15
Kutumia vyungu vitatu	16
Mashapo kwa Kemikali	18
Usafishaji kwa chujio	20
Kinara chujio	20
Mchanga chujio	21
Kuhifadhi vyema na kutumika	22
Kukuza kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani kwa kila nyumba	24
Muundo wa maamuzi ya kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani	27
Vijikaratasi vya maelezo	30
Kutumia vyungu vitatu	30
Jinsi ya kutibu maji kwa WaterGuard (Sur'Eau)	32
Jinsi ya kutibu maji kwa tembe za klorini	34
Jinsi ya kutibu maji kwa Watermaker	36
Jinsi ya kutibu maji kwa vifurushi vya PUR	38
Habari zaidi	40



Ubora wa Maji kwa Ufupi

> Kwa nini ubora wa maji ni muhimu?

Maji safi ni muhimu sana kwa watu na kwa afya njema, hasa wakati wa dharura.

> Maji huchafuliwaje?

Maji yanaweza kuchafuliwa katika vyanzo, nyumbani, au wakati wa usafirishaji kutoka vyanzo hadi nyumbani.

Vyanzo vya maji visivyolindwa vyema, chombo kichafu, au mikono isiyooshwa yote yanaweza kuchafua kugeuza maji, hata maji yanayoonekana kuwa ni safi na yana ladha nzuri, na kuwa ya kuleta magonjwa kwa watu.

Maji yanaweza kuchafuliwa kwa njia nyingi, kama vile:

- Matangi ya maji machafu na vyoo.
- Maji machafu ya mitaro yanayoingia katika visima na chemchemi ya maji.
- Kuchota maji kwa mikono michafu isiyooshwa na vyombo vichafu.
- Wanyama pia kutumia vyanzo hivyo hivyo.
- Vitu kuanguka kuangukia visimani.

Kwa hali yoyote, maji katika vyanzo ni hatua moja tu ya mfululizo ya maji???? Hata maji safi yaliyochotwa kutoka vyanzo yanaweza kuchafuliwa kabla ya kutumika kwa sababu za tabia chafu za wanaoyatumia kama vile:

- Kutumia vyombo vichafu vya maji kusafirisha maji nyumbani kutoka vyanzo.
- Kuhifadhi maji nyumbani katika vyombo wazi na /au vyombo vichafu vya maji.
- Kutumia maji nyumbani kwa vyombo vichafu au mikono michafu.



Kila kiwango katika mfululizo huu kinaweza kuwa ni nafasi ya maji kuchafuliwa.

> Ni ubora gani wa maji tunaotaka?

Kuna sababu nyingi za kuboresha ubora wa maji. Muhimu sana ni kuondoa viumbe kama viini vya uchafu chafu na vimelea vinavyoleta magonjwa. Pia tunaweza kutaka kuondoa vitu vinavyoning'inia kama chafu vinavyofanya maji kuonekana kuwa chafu na kuwa na ladha mbaya na pia vinaweza kubeba viini vya chafu vinavyoleta magonjwa kwa watu.

> Ni ubora gani wa maji haujaguzwa na mwongozo huu?

Maji yanaweza kuwa hatari kwa afya yakiwa yamebeba vitu vingine, kama dawa zinazotumika kwa ukulima au mengine yanayosanyika kwa kawaida. Au, kama chuma, yanaweza kuwa salama kuyanywa lakini yana ladha mbaya sana inayofanya watu kuyatafuta maji mengine yanayo ladha nzuri lakini yanawaleta magonjwa.

Habari kuhusu mambo kama haya yanaweza kupatikana kwingine (tazama kurusa za Habari zaidi).

> Nitajuaje kukiwa maji yamechafuliwa?

Kuna njia nyingi za kupima ubora wa maji. Yote yanahitaji vifaa na / au kemikali. Kupima ubora wa maji haujaguzwa katika kitabu hiki cha mwongozo. Maelezo zaidi yanapatikana katika kurasa za habari zaidi.

Kukiwa kupima kwa ubora wa maji hauwezekani, vyanzo na mienendo ya watumiayo inaweza kuchunguzwa ili kutambua hatari zilizoko kwa afya ya binadamu.

1	Je, watu wanateka maji kutoka kwa pampu au bomba vyema wima?		
2	Je, pampu yenyewe au mfumo wa maji uko katika hali nzuri?		
3	Je, maji yenyewe yanaonekana ni safi?		
4	Je, sehemu iliyo karibu na pampu ni safi?		
5	Je, watu wanazingatia matumizi ya maji safi na uhifadhi wa maji safi?		
6	Je, watu wanazingatia tabia nzuri za usafi		

Kukiwa jibu la swali lolote ni LA, kuna uwezekano kwamba kuna shida na ubora wa maji.

Katika hali ya dharura, watu watakuwa na uwezo wa kupata viini vinavyoleta magonjwa. Kukiwa na rasilimali za kutosha, ni bora zaidi kujitahadhari na kusaidia hata wale walioa na maji safi ili kupunguza hatari za mlipuko.

> Ubora wa Maji kwa Ufupi

Utangulizi wa kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani

> Je, kutibu maji ya nyumbani ni nini?

Kutibu maji ya nyumbani ni shughuli yoyote ile ya kuboresha ubora wa maji katika kiwango cha nyumbani.

> Je, kuhifadhi vyema maji ni nini?

Kuhifadhi vyema maji ni kutumia vyombo safi vilivyo na vifuniko NA tabia nzuri za usafi zinazozuia uchafuaji wakati wa kuteka maji, usafirishaji na kuhifadhi nyumbani.

> Je, kwa nini tunakuza kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani?



Ni bora daima kutumia maji yaliyotoka kwenye chanzo safi na yaliyohifadhiwa vyema. Kwa hali yoyote, haya hayaweze kila wakati, hasa wakati wa dharura. Labda kuna uchafuaji wa chanzo unaofanya chanzo kutotumika. Au idadi ya watu wengi hawana vyombo safi au hawazingatii tabia nzuri za usafi.

Njia moja ya kupambana na shida hii ni kutibu maji ya nyumbani. Haya ni njia za muda mfupi tu hadi vyanzo vya maji viboreshwe. Mbinu za kutibu maji nyumbani zinaweza kutekelezwa na mtu wowote wa familia baada ya kupata mafunzo mafupi kuhusu mbinu hizi.

Juhudi za kuboresha ubora wa maji ya nyumbani yana athari kubwa kwa afya na zinaweza kufikia idadi kubwa kwa muda mfupi.

> Je, kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani yanafanywaje?

Kitabu hiki cha mwongozo kinaeleza njia nyingi za kutibu maji ya nyumbani na ina maelezo ya matumizi yao.

Ni muhimu sana kwamba watu wanaopokea vifaa vya kuitikia hali za dharura wajue kutumia vifaa hivyo. Kuna miongozo mbali mbali kwa bidhaa mbali mbali za kutibu maji ya nyumbani na kwa bidhaa zinazokuja kwa kiwango wa ukubwa mbali mbali. Ili kuwa mzoefu wa bidhaa za kutibu kabla ya usambazaji kuanza. *Jaribu bidhaa wewe mwenyewe.* Hakikisha kwamba hakuna mtu wowote anayepokea kitu, kiwe kemikali au mtungi, bila kujifunza jinsi ya kuitumia.

Ushirikiano na kuwa wa karibu na timu ya usambazaji ni muhimu sana kulingana na gharama za baadhi hizi na hatari za kunywa maji yaliyochafuliwa.

Kitabu hiki cha mwongozo pia kinajumuisha msingi wa mwongozo jinsi ya kuhusisha usambazaji wa bidhaa katika hali za dharura na kukuza shughuli za tabia ya usafi kuhusu matumizi mema na uhifadhi katika kiwango cha nyumbani.

> Je, kutibu maji ya nyumbani ni salama?

Usalama halisi upo kwa kila awamu. Kwa kweli, mbinu na bidhaa zinazoelezwa katika kitabu hiki cha mwongozo ni salama. Kwa hali yoyote, sharti umakini unafaa uwe kunapo tumika kemikali, hasa kukiwa na watoto.

> Je, maji kiasi gani yanahitajika kutibiwa?

Kiasi inayotosha tu.

Maji safi mara nyingi hayapatikani wakati wa dharura na njia zote za kutibu zilizotajwa katika kitabu hiki cha mwongozo zina gharama kifedha na wakati au zote mbili. Maji kidogo zaidi yanayohitajika kutibiwa ni yale ya kunywa na yale yanayotumika kutayarisha vyakula visivyopikwa. Kwa kawaida ni kama lita 5 (tano) kwa kila mtu kwa siku yanahitajika. Lakini haya yanategemea hali ya hewa na idadi ya watu.

Kukiwa maji yasiyotibiwa yanaonekana ni angavu ya kutosha, si kwa kawaida yatahitaji kutibiwa kabla ya kutumika kwa kazi za nyumbani kama kuoga na kufua.

> Kuna njia gani za kutibu?

Kitabu hiki cha mwongozo kitaangaza njia tatu za kutibu maji:

- Usafishaji – kuhakikisha kwamba maji hayana viini vinavyosababisha magonjwa. Haya yanaweza kufanyika kwa njia za kemikali, moto, na hata miale ya jua.
- Mashapo – kukubali chafu kutulia chini ya chombo cha maji kwa muda.
- Safisha kwa chujio – kutoa chafu moja kwa moja kwa kupitisha maji katika kifaa kama finyanzi au mchanga.

> Nitachaguaje njia ya kutibu?

Tazama Muundo wa maamuzi ya kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani iliyo katika kitabu hiki cha mwongozo kwa njia za moja kwa moja za kuchagua njia ya kutibu.

Uamuzi wa njia ya kutibu utategemea ni wapi na ni hali gani ya dharura. Labda hakutakuwa na jibu moja sahihi au suluhu ya kufaa. Wakati mwingine chaguo ni yale yaliyoko. Na jambo muhimu sana, ni watu wanaoenda kutumia njia ya kutibu au bidhaa lazima wahitaji kuitumia.

> Taratibu za kutibu maji ya nyumbani

> Kupitisha kwa kichujio

Kupitisha maji kwa kichujio ni hatua muhimu ya kwanza, kufanywa sawa sawa, kutaboresha utendaji wa taratibu zote zilizotajwa katika kitabu hiki cha mwongozo.

Kumimina maji ya matope au maji yanayoonekana ni machafu katika kitambaa kizuri, safi cha pamba mara nyingi kutatoa idadi ya chafu na vijidudu vilivyoko majini.

Jaribio la kujua kama kitambaa kinafaa ni kukitumia kuchujia maji. Kukiwa chafu hazipenyi kitambaa, basi kitambaa kinafaa kwa chujio. Kitambaa cha pamba kinafaa zaidi na haufai kuona upande ule mwingine kwa kupitia kitambaa. Pia kitambaa hakifai kuwa kigumu sana kupitisha maji na kuchukua muda mrefu.

Kufua kitambaa kati ya matumizi kutafanya kuchujia kuwa rahisi na wa kufaa.

Kuchujia maji pekee yaliyotoka kwenye chanzo kilichochafuliwa hayafanyi maji kuwa salama kwa kunywa, lakini kunarahisisha kutibu maji ya nyumbani.



> Usafishaji

Kukiwa maji yanaonekana ni angavu lakini yawezakuwa yamechafuliwa, lazima yasafishwe.

Kitabu hiki cha mwongozo kitaeleza njia tatu za usafishaji:

- Kuchemsha.
- Nguvu za jua.
- Usafishaji kwa kemikali.



Usafishaji mara kwa mara unaweza kubadili ladha ya maji.

- Kuchemsha maji kutayaacha maji bila ladha yoyote.
- Nguvu za jua yatayaacha maji kuwa moto.
- Kemikali yatayaacha ladha kali na mbaya.

Shida hizi zote zinaweza kumalizwa kwa njia rahisi. Ni muhimu kuzungumza na watu wanaotumia njia hizi kuhusu haya ili kuhakikisha kwamba hawaachi maji safi na kutumia maji kutoka vyanzo vichafu au kuacha kutibu maji wanaoyateka

> Kuchemsha

Kuchemsha maji ni njia ya kienyeji kutibu maji. Kukifanywa vizuri kunaweza kutoa maji safi kwa idadi ya watu wasio na njia nyingine.

Kuchemsha kuna uzuri na ubaya.

- ▲ Kuchemsha maji kutaua viini vyote vinavyosababisha magonjwa
- ▲ Kuchemsha maji kunaweza kufanywa na watu wenyewe
- Inachukua kilo moja ya kuni kuchemsha maji lita moja kwa dakika moja. Kuchemsha hakufai kukuzwa katika sehemu ambazo zina uhaba wa kuni ila na hakuna njia zingine za kuchemsha maji.
- Kuchemsha maji hakutaondoa povu povu.
- Kuchemsha maji hakuzuii milele, kwa hivyo kutohifadhi vyema kutasababisha kuchafuliwa tena. Maji yaliyochemshwa yanafaa kuhifadhiwa vyema na kutumiwa upesi kwa siku chache sana.



Kuchemsha kunafaa kukiwa na moto ya hali ya juu sana. Maji ya mvuke tu siyo maji yaliyodheruka na kuchemka.



Kuchemsha kufanya kazi lazima maji yenyewe kudheruka na kutoa viputo.



> Nahitaji kuchemsha kwa muda gani?

Kukiwa maji ni kwa chini mekoni *dakika moja ya kudheruka na kutoa viputo.*

Kukiwa maji ni kwa juu mekoni *dakika tatu ya kudheruka na kutoa viputo.*



Dokezo


Kuchemsha maji kutayaacha maji bila ladha yoyote. Kwa hali yoyote, haya yanaweza kubadilishwa kwa kutingiza maji kwa chupa au mtungi mdogo au kuongeza chumvi kidogo sana kwa kila lita ya maji yaliyochemshwa

> Usafishaji kwa nguvu za jua

Kuweka maji kwa miale ya maji kutaua viini vinvyosababisha magonjwa. Haya yanatumika sana kukiwa joto ni hali ya juu sana (ingawaje joto ya maji haitajiki kuwa ya juu kuliko 500C).

Njia moja rahisi ya kutibu maji ni kuziweka chupa za plastiki za maji au glasi za maji kwenye jua. Katika nchi za tropiki, hali bora za kuziweka kwenye jua ni kwa masaa matano hivi katika jua la aduhuri.

Wakati wa kuziweka chupa kwenye jua utaongezeka (kwa siku mbili badala ya moja) kukiwa maji yenyewe yana povu povu. Kuwekwa kwa jua pia kutaongezeka kukiwa hakuna jua ya kutosha (msimu wa mvua).




> Nitatumiaje usafishaji kwa nguvu za jua?

Njia hii, pia inajulikana kama mfumo wa SODIS, inatumia chupa za plastiki au glasi zisizokuwa na rangi au ni angavu kuongeza joto ya maji kwa kuziweka moja kwa moja mjoa kwenye miale ya jua.

Kwa matokeo bora zaidi weka chupa katika paa la mabati

Maji pia yanaweza kuwekwa kwenye mfuko wa plastiki usiokuwa na rangi au ni angavu kukiwa hakuna chupa.



Dokezo

Kuharakisha namna ya hali, tia maji thuluthu ya chupa kisha tingiza sana. Halafu jaza chupa kabisa na kuiweka kwenye miale ya jua. Kuitingiza mara kwa mara wakati chupa iko kwenye jua pia kutasaidia sana.

**Dokezo**

Watu hawatapenda kunywa maji moto, au maji yaliyotibiwa. Wahimiza waache maji kupoa kisha wanywe

Usafishaji kwa nguvu za jua una uzuri na ubaya.

- ▲ Usafishaji kwa nguvu za jua utaua viini vyote vinavyosababisha magonjwa kukiwa kutawekwa kwenye jua kwa muda mrefu wa kutosha.
- ▲ Usafishaji kwa nguvu za jua unaweza kufanywa na watu wenyewe kwa kutumia vifaa vilivyoko kote (chupa au mifuko ya plastiki isiokuwa na rangi au ni angavu).
- Usafishaji kwa nguvu za jua hauzui milele, kwa hivyo kutohifadhi vyema kutasababisha kuchafuliwa tena. Maji yaliyosafishwa kwa mbinu hii yanafaa kuhifadhiwa vyema na kutumiwa upesi kwa siku chache sana.
- Usafishaji kwa nguvu za jua unachukua muda mrefu kuliko mbinu hizo zingine na pia unahitaji msimu wa jua.

> Usafishaji kwa kemikali



Kuna kemikali aina nyingi kwa usafishaji wa maji. Hizi kemikali zina tofauti zao kulingana na matokeo yao na usalama wao.

Shirikisho la Kimataifa hasa hutumia tembe za klorini kwa usafishaji wa maji ya nyumbani katika hali za dharura.

> Nitatumiaje kemikali kwa usafishaji ?

Jinsi ya kutibu maji kwa kutumia tembe za klorini




Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.



Je, maji yako yanaonekana ni angavu?



Weka tembe moja kwa mtungi safi kisha funika mtungi.



Ngoja kwa dakika thelathini.



Maji sasa ni tayari




Je, maji yako yanaonekana ni chafu?



Chujia maji yako kwa kupitisha maji kwa kitambaa kisafi.



Ongeza tembe mbili kwa mtungi kisha funika mtungi.



Ngoja kwa dakika thelathini.



Maji sasa ni tayari

Klorini ya maji ya WaterGuard

WaterGuard (pia inajulikana kama Sur Eau) pia ni klorini ya maji. Ina nguvu sawa kama klorini za tembe.

Klorini ya maji ya WaterGuard

Je, maji yako yanaonekana ni angavu?

Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.

Ongeza kifuniko kimoja kwa mtungi wa maji wa lita 20, kisha funika mtungi.

Ngoja kwa dakika thelathini.

Maji sasa ni tayari

Je, maji yako yanaonekana ni chafu?

Chujia maji yako kwa kupitisha maji kwa kitambaa kisafi.

Ongeza vifuniko viwili kwa mtungi wa maji wa lita 20, kisha funika mtungi.


Ngoja kwa dakika thelathini.

Maji sasa ni tayari



Uangalifu lazima kuzingatiwa wakati wa kutumia kemikali. Usiweke kemikali kwa macho yako. Kemikali lazima ziwekwe mbali na watoto na pahali pakavu pasipokuwa na jua. Bidhaa hizi huwa na maelezo ya mwongozo katika pakiti. Kwa hali yoyote, maelezo yanaweza kuwa kwa lugha ambayo watu hawatumii au hawawezi kuyasoma.

Hakikisha watu wote wanaopokea kemikali wamepata mafunzo na wanajua kutumia kemikali. Tazama kurasa za Kukuza Kutibu na Kuhifadhi Vyema Maji ya Nyumbani kwa maelezo zaidi. Kwa sababu za ubora na kupatikana kwa kemikali kwa wingi, kemikali nyingi kama za kufua hazifai kutumika kwa usafishaji wa maji ila ijapokuwa hakuna njia nyingine na mafunzo mema na usimamizi kuwepo.



Dokezo

Usafishaji kwa kemikali sio bora sana kukitumika kwa maji chafu au maji ya povu povu. Kukiwa maji yaonekana ni chafu au yana povu povu, tumia kemikali mara mbili zaidi.

Dokezo

Dokezo: Usafishaji kwa kemikali, hasa mara mbili zaidi, kuweza kuacha ladha ambazo watu hawapendi. Hali kama hii inaweza kuwafanya waache kutibu maji. Shida ya ladha inaweza kuondolewa kwa kutumia idadi ya kemikali inayotosha na kwa kutingiza maji kwenye chupa ili kuongeza hewa majini

Dokezo

Zungumza na watu kuhusu bidhaa. Je, ni rahisi kuitumia? Je, ina ladha gani? Labda bidhaa tofauti inatakikana (tazama sehemu inayofuata).

Dokezo

Kuacha mtungi wazi bila kufunika na kuuacha kwenye joto (kwa mfano kwenye miale ya jua) kutapunguza nguvu za kemikali kulinda dhidi ya kuchafuliwa. Himiza watu kuhifadhi maji kwa kufunika na kuweka mbali na jua kukiwezekana.

Usafishaji kwa kemikali kuna uzuri na ubaya.

- ▲ Bidhaa hizi ni rahisi na salama kutumia.
- ▲ Kuna nguvu za usafishaji badaye inayolinda dhidi ya uchafuliwaji baada ya kutibu.
- Bidhaa hizi lazima kuletwa kutoka nje ya jamii; siyo jambo wanaloweza kwa rasilimali zao.
- Usafishaji kwa kemikali hautaondoa viini vyote vinavyosababisha magonjwa. Maji yanafaa kuchujiwa kabla ya usafishaji kwa kemikali kutumika ili kuhakikisha kwamba hatari zote zimeondolewa.

> Mashapo

Kukiwa maji yana matope, kuyapatia muda kutulia au kuongeza kemikali kunaweza kufanya chafu kuanguka chini ya mtungi na kuacha maji kuwa angavu. Kuchuja maji kwa kitambaa kunaweza kufanya kurahisisha utaratibu huu na kupata matokeo mema.




Kumbuka: Maji yaliyofanywa kuwa angavu kwa mashapo si safi. Bado yanahitaji usafishaji ilikuondoa viini vinavyosababisha magonjwa. Lakini kuyafanya maji kuwa angavu yanayafanya kuwa rahisi kwa usafishaji.

> Kutumia vyungu vitatu

> Kutumia vyungu vitatu reverse the order

Nitatumiaje vyungu vitatu?



Kila siku maji yanapoletwa nyumbani:

- A Kunywa maji kutoka mtungi wa tatu (3).
- B Kwa utaratibu tia maji yaliyo kwenye mtungi wa pili (2) kwenye mtungi wa tatu (3)
- C Osha mtungi wa pili (2)
- D Kwa utaratibu tia maji yaliyo kwenye mtungi wa kwanza (1) kwenye mtungi wa pili (2)
- E Osha mtungi wa kwanza (1)
- F Tia maji yaliyotekwa kutoka chanzo cha maji (ndoo nambari nne 4) kwenye mtungi wa kwanza (1) pitisha kwa chujio kukiwezekana.

Acha maji kutulia kwa siku moja kisha rudia taratibu tena.

Kunywa maji tu kutoka kwa mtungi wa tatu (3). Maji haya angalau yamehifadhiwa kwa siku mbili, na ubora wake umeongezeka. Baada ya muda wa siku kadhaa mtungi huu utasafishwa kwa maji moto sana.

Kutumia tiubu ya mpira au bomba la mpira kufyonza maji kutoka kwa mtungi ni bora kwa sababu maji hayachafuki sana kama kutia.



Dokezo

Njia hii inaweza kuboreshwa kwa kutumia kitambaa cha kuchujia kila unapotia kwenye mitungi.

Dokezo

Kutumia vyungu vitatu ni njia nzuri kwa muda mfupi inayoweza kuwako wakati wa dharura hadi njia zingine ziweko au ubora wa chanzo cha maji kuimarishwa.

Dokezo

Katika hali ya dharura, watu labda hawana mitungi mitatu. Ingawa haitakuwa sawa kama ilivyoelezwa hapo juu, mitungi miwili bado ni sawa badala ya mitatu. Wakati utahitajika zaidi ili kuacha chafu kutulia na viini vinavyosababisha magonjwa kufa.

Kuna uzuri na ubaya kutumia vyungu vitatu.

- ▲ Njia ya kutumia vyungu vitatu inapunguza chafu sana na kuua viini vinavyosababisha magonjwa katika maji.
- ▲ Njia hii haina gharama kubwa, ni rahisi kutumia na watu wanaweza kufanya wao wenyewe kwa kutumia rasilimali zinazopatikana.
- Njia hii inapunguza, lakini haiondoi viini vyote vinavyosababisha magonjwa . Kusafisha kwa kuchemsha, kutumia kemikali au kutumia nguvu za jua bado zahitajika kuondoa hatari zote za magonjwa.

> Mashapo kwa kemikali

Mashapo kwa kemikali ni kutumia kemikali kuharakisha kutoa chafu kwa maji.

Bidhaa mbili za mashapo kwa kemikali zinazotumika sana na Shirikisho la Kimataifa la Shirika za Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu wakati wa dharura ni PUR na Watermaker.



Gramu tano kwa kila lita 20



gramu mbili unusu kwa kila lita 10




gramu nne kwa kila lita 10

Kemikali hizi ni muhimu hasa wakati wa mafuriko, kwa sababu zinaondoa chafu kutoka kwa maji NA kusafisha. Zote mbili ni bora kwa matumizi ya kutibu maji ya nyumbani wakati wa dharura na Shirikisho la Kimataifa la Shirika za Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu haipendekezi bidhaa nyingine kuliko nyingine.

> Je, inafanyaje kazi?

Bidhaa hizi huwa na kemikali aina mbili pamoja. Kemikali moja inafanya kazi kama gamu na inafanya chembe ndogo ndogo kushikana pamoja. Hii inatengeneza chembe kubwa, inayoitwa kibonge, kinachoanguka chini mtungini kwa haraka.



Halafu kemikali nyingine inasafisha maji angavu, kama vile mashapo kwa kemikali ilivyoelezwa hapo awali katika kitabu hiki cha mwongozo.

> Kukiwa zinafanya mara mbili zaidi, kwa nini daima hatutumii bidhaa hizi?

Bidhaa hizi ni ghali zaidi na ni ngumu kuzitumia kuliko njia hizo zingine. Kwanza kukiwa maji ni angavu au yenye povu povu kidogo na, pili usafishaji kwa kemikali kunawekana, basi usitumie mashapo kwa kemikali.


> Nitatumiaje mashapo ya kemikali?



Teka maji




Kusanyika kwa kibonge chini ya mtungi baada ya kemikali kuwekwa



Kibonge kinakuwa baada ya kukorogwa



Kubadilisha maji kuto-ka mtungi mmoja hadi mtungi mwingine kwa kutumia kitambaa safi cha pamba kwa kuchujia



Maji safi tayari kuhifadhiwa na kwa matumizi

Dokezo

Kutumia ndoo angavu kwa maonyesho kunawaonyesha vikundi jinsi bidhaa inafanya kazi. Lakini fanya vikundi vidogo ili kila mtu ajifunze.

Dokezo

njia hii inaweza kuboreshwa kwa kutumia kitambaa chujio maji yanapotiwa kwenye mitungi.

Paketi moja ya PUR hutumika kwa kutibu lita 10 ya maji. Watermaker inakuja kwa paketi tofauti na inatibu idadi tofauti ya maji. Tazama paketi, bidhaa hizi huwa na maelezo kwenye paketi kabla ya kufunza watu jinsi ya kuitumia.

Mashapo kwa kemikali ina uzuri na ubaya.


- ▲ Bidhaa hizi zinafanya maji ya matope kuwa salama na kunywa.
- ▲ Kuna nguvu za usafishaji badaye inayolinda dhidi ya uchafuliwaji baada ya kutibu.
- Bidhaa hizi ni ngumu kutumia na zinahitaji mafunzo zaidi na mfuatilio.
- Bidhaa hizi ni ghali sana kwa kila lita ya maji yanayotibiwa kuliko bidhaa za usafishaji kwa kemikali na itumike tu kukiwa maji ni ya matope au bidhaa nyingine yoyote haiko.
- Watu watahitaji zaidi ya mtungi moja kutumia hizi kemikali kwa njia nzuri.

➤ Usafishaji kwa chujio

Chujio linatoa chafu kutoka kwa maji kwa kuzizuia na kuachilia maji kupita. Maji yanapitia kifaa kama mchanga au ufinyanzi na vitu hatari zinashikwa kwenye chujio.

Chujio halitumiki sana wakati wa dharura. Yatajulishwa tu na kueleza kwa ufupi. Maelezo kamili kuhusu chujio, yapatikana kwa habari kutoka kurasa zingine (tazama Habari zaidi).

➤ Kinara chujio



Kinara chujio zinatengenezwa kwa ufinyanzi. Maji yanatiliwa kwenye mtungi mmoja na yanapitia ufinyazi polepole hadi mtungi mwingine

Chujio linapanguzwa na burashi mara tu chafu inamiminika kwenye chujio na kutiririka kwa maji kati ya mitungi kunapungua.



Kukiwezekana chujio pia linafaa kuchemshwa ili kua viini vinavyosababisha magonjwa vilivyokwama kwenye chujio.

Ikiwa maji ni chafu ndiyo vile chujio linazidi kupanguzwa. Mwishowe kinara kitaisha polepole kwa sababu ya kupanguzwa na lazima kibadilishwe.

Kinara chujio kina uzuri na ubaya.

- ▲ Bidhaa hizi ni rahisi na salama kutumia.
- ▲ Kukitunzwa vyema, bidhaa hii inaweza kutumika kutoa maji safi kwa muda mrefu
- Bidhaa hizi mara nyingi ni ghali na ni rahisi kuvunjika.
- Inaweza kuchukua muda mrefu kutibu maji, hasa maji yakiwa machafu sana.
- Hakizui uchafuaji wa maji milele, kwa hivyo mtungi wa maji safi lazima kufunikwa ili kusiwe na uchafuaji.
- Bidhaa hizi zinahitaji utunzaji wa kila mara na pia zinahitaji mafunzo na mfuatilio.



> Mchanga chujio

> Kutibu cha mbele

Kuchuja kwa kutumia mchanga ni chaguo la kutibu cha mbele rahisi na haraka inayopunguza idadi ya maji machafu na kufanya usafishaji kuwa na matokeo mema kamili.

Watumiaji wanatia maji kutoka kwa mtungi mmoja kwa kupitia mtungi ulio na mchanga na una shimo au mrija chini. Halafu maji yanatiririka kwa mtungi wa kuyahifadhi.


Kutibu cha mbele kutumia mchanga kuna uzuri na ubaya.

Mbinu hii ni rahisi na haraka kutumia.

Ni nzuri kwa matokeo ya kuondoa chafu na viini vinavyosababisha magonjwa. Hii inawezesha njia hizo zingine za kutibu maji kuwa na matokeo kamili.

Si ghali kukiwa mchanga na mitungi inaweza kupatikana eneo hilo.

Inahitaji mitungi mitatu na mrija.




> Mchanga-hai chujio

Ingawa haitumiki sana kwa hali za dharura, mchanga-hai chujio ni njia bora zaidi na wa kudumu kwa kutibu maji ya nyumbani. Mchanga-hai chujio linachuja maji kwa kupitishia mchanga na NA vimelea vilivyoota kwenye chujio. Chujio huoshwa tu ikiwa limechafuka na maji hayapitii.

Kwa sababu vimelea vinahitaji muda kuota, chujio halitatibu maji vizuri mara ya kwanza likitumika na mara tu baada ya kuoshwa.

Ingawa chujio haya ni rahisi kutumia, yanahitaji ujuzi wa mafunzo yanapogawiwa. Habari za ujenzi na utunzaji wa chujio haya yanaweza kupatikana katika kurasa za habari zaidi.

- ▲ Kukitunzwa vizuri, chujio hili linaweza kutibu maji kwa muda mrefu sana.
- Linaweza kuchukua muda mrefu sana kutibu maji, hasa maji kukiwa chafu sana.
- Hayazui uchufuaji wa maji milele, kwa hivyo mtungi wa maji safi lazima kufunikwa ili kusiwe na uchufuaji.
- Bidhaa hizi zinahitaji utunzaji wa kila mara na pia zinahitaji mafunzo na mfuatilio.



> Kuhifadhi vyema na kutumika



Juhudi zote za kutibu maji ni bure kukiwa maji yanahifadhiwa kwa njia mbaya na kutumiwa vibaya.


Lakini kuna shida

Mitungi yenye shingo mirefu inazuia uchafuaji lakini ni shida kusafisha.

Mitungi yenye shingo pana ni rahisi kwa uchafuaji lakini ni rahisi kusafisha.

Katika hali za dharura, watu watumia mitungi waliyonayo au mitungi watakayopewa wakati wa usaidizi, au zote mbili, tumia utakayopata.

Himiza watu waweke mitungi safi, iliyofunikwa na mbali na watoto. Ni bora zaidi kukiwa watu wanatumia mitungi tofauti kwa kuteka maji na kuhifadhi maji.



Kwa mitungi iliyo na shingo mirefu, himiza watu waisafishe kila mara kwa kutumia sabuni ya maji, usafishaji kwa kemikali, au kutumia changarawe.

Kwa mitungi iliyo na shingo pana, himiza watu kuifunika na kubuni njia ya kuchota maji bila mikono yao kuyaguza maji, watumie ukasi mrefu unaowaruhusu kuchota bila kuyaguza maji au mrija chini ya mtungi. Pia wahimizwe kuisafisha mitungi yao kila mara.

Hata baada ya ubora wa chanzo cha maji kuboreshwa, juhudi za kuwaeleza kuboresha uhifadhi na kutimika kwa maji itafaidisha afya ya watu.

Himiza watu wanawe DAIMA na kila wakati kabla ya kutumia maji ya kunywa. Usambazaji wa kemikali za kutibu maji ni nafasi kubwa ya kugawa sabuni na kutoa maarifa na ujumbe wa usafi.



> Kuhamasisha kwa kila nyumba

Kukuza kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani kwa kila nyumba



> Mafunzo

Kemikali haifai KAMWE kusambazwa bila watu kufunzwa matumizi yao. Kabla ya usambazaji wa kemikali, panga namna mafunzo yatafanywa. Inapendekezwa kwamba mafunzo ya kemikali ya-jumuishwe pamoja na shughuli ya kujulisha usafi unaotajwa hapa chini.

Maelezo ya kemikali za kutibu huwa za ukubwa wa kawaida, kwa mfano mitungi ya lita 20, au ndoo za lita 10(tazama vijikaratasi vya maelezo). Watu wanaweza kuwa wakitumia mitungi ya kienyeji ya ukubwa tofauti tofauti kwa mifano, vyungu vya lita 14. Washirikishe ili kupata kipimo wanachoelewa na wanaweza kuendelea nacho wao wenyewe.

Kukiwa watu hawajui bidhaa, hasa kemikali, swali la uaminifu linaweza kuzuka. Njia moja ya kusuluhisha swali hili ni kufanya jaribio kwa kutumia bidhaa wewe mwenyewe hadharani.

Unapotoa mafunzo, fanya jaribio la bidhaa kwanza ili kuwa na wakati wa kutosha kwa klorini kufanya kazi au chujio kusafisha maji ya kutosha ili uyanywa hadharani.

> Kukuza shughuli za tabia za usafi

Kusamabaza tu kemikali kwa watu hakutaboresha afya zao. Kuwafanya watu kutekeleza kutibu na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani ni njia ya kubadili tabia.

Kendo na imani ya wengi, mabadiliko ya uzoefu au tabia haichukui muda mrefu kufanyika na hata mabadiliko ya muda mfupi ni muhimu panapo hatari kubwa kwa afya. Kukiwa watu wenyewe wanahisi wamo hatarini, wanaweza kuwa wepesi sana kubadili tabia zao.

Kwa hivyo, kukiwa imani ya kubadilika imewezeshwa, kubadilika itakuwa haraka sana. Kwa mfano, mitungi ya maji yakitolewa kurahisisha jamaa kuhifadhi maji kwa njia nzuri nyumbani. Sisitizo lazima iwe kuwezesha wanawake, wanaume na watoto kuchukua hatua kupunguza hatari za afya. Yaani, watu wawe na tabia njema ya usafi kuliko kujulishwa vyanzo vya magonjwa.

Katika hali za dharura, jambo muhimu linaloleta mabadiliko makubwa ni faida ya afya. Lakini hili silo jambo pekee. Ni muhimu kutambua utamaduni / mila ya kawaida ya jamii inayoweza kuwa motisha kwa kubadili tabia. Kwa mfano, mama anaweza kuiga njia ya kutibu maji kutoka kwa jirani wake baada ya kumwona akiitumia.

Kutoa vitu vya usafi kwa watu pia inaweza kuwavutia kushiriki katika shughuli za kukuza usafi.

Vifaa vingi vimo kwa matumizi ya kukuza utiifu wa tabia za usafi katika hali ya dharura. (tafadhali tazama kurasa za Habari zaidi).



Usamabazaji wa kemikali za kutibu maji ya nyumbani ni nafasi nzuri ya kusamabaza sabuni na vitu vingine vinvyohusu maji na Vitu Visivyo Chakula (VVC) kwa usafi na kupasha ujumbe muhimu kuhusu matumizi na kuhifadhi vyema maji. Nafasi muhimu ya kuwezesha afya bora na usafi unaweza kutokuwa kukiwa watu hawajapashwa habari kamili kuhusu faida za vitu vilivyosamabazwa.

Hatua nne za kwanza kutekeleza ukuzaji wa tabia za usafi katika hali ya dharura:

1. Fanya makadirio yanayolenga maji, taka na usafi

Maji					Usafi wataka	Usafi
Chanzo cha maji	Kutekamaji na usafishaji	Kuhifadhi maji	Kutibu maji	Matumizi ya maji	Kutumia vyoo	Kunawa
1 Vyanzo vya maji vinafaa vitumiwe kwa uangalifu na kukiwa kwa hali nzuri.	3 Maji ya kunywa yanafaa kuwekwakutekwa kwa vyombo safi, bila mikono kuyaguza maji.	5 Maji yanafaa kuhifadhiwa kwa vyombo safi vinavyofunikwa na kusafishwa kila mara.	7 Taratibu za kutibu maji zinafaa kutekelezwa katika kila nyumba kukiwa chanzo si safi na maji hayajahifadhiwa vyema.	8 Maji ya kunywa yanafaa kuchotwa kutoka chombo cha kuhifadhi kwa kutumia ukasi ili mikono, vikombe na vyombo vingine visichafue maji.	9 Vyoo vinafaa kutumika badala ya kuenda haja ovyo ovyo kila pahali	12 Makazi yanafaa kuwa na sabuni au jivu na maji ya kunawa mikono.
2 Haifai kuwa na hatari ya uchafuaji kutoka vyoo vya karibu, maji taka, wanyama na vitu kuanguka visimani	4 Maji yanafaa kusafirishwa kwa vyombo vilivyofunikwa.	6 Maji ya kunywa yanafaa kuhifadhiwa kwenye chombo tofauti na vyombo vya maji ya matumizi ya kawaida nyumbani			10 Vyoo vinafaa viwe mbali na vyanzo vya maji na viwe safi kila wakati.	13 Watu wanafaa kunawa mikono yao kwa wakati unaofaa.
					11 Mashimo yanafaa kuzolewa au kubadilishwa mara kwa mara.	

2. Chagua makundi yanayokusudiwa

Mwanzoni mwa hali ya dharura, mara nyingi tunafanya kampeni bila kuwa na makundi maalumu yanayokusudiwa. Inapendekezwa kwamba tutambue watu maalumu husika ili tuelekeze ujumbe kwa makundi husika kwa kutekeleza shughuli zinazotajwa.

Kwa mfano, kukiwa ni watoto ndio wanahusika kuteka maji, hao ndio wanafaa kusudiwa na ujumbe wa tabia za utekaji na tabia za usafirishaji wa maji .

3. Anzisha ujumbe wa usafi

- A Ujumbe unafaa kulenga mambo machache muhimu: kukiwa ni mfupi ni bora! Kuchosha watu na ujumbe unaweza kuleta matokeo mabaya.
- B Toa ujumbe kwa matokeo bayana na tumia ucheshi wa kutosha.
- C ujumbe wa kukuza usafi unafaa kuwa wa rahisi kwa maneno ya lugha inayotumika

Kukiwezekana fanya jaribio la ujumbe kwa kutumia kundi la walio na rika moja, kiwango cha elimu sawa na utamaduni moja ambao ujumbe unawalenga.



4. Chagua njia za mawasiliano

Chaguo la njia za mawasiliano linategemea aina ya watu na rasilimali inayotumika. Katika hali za dharura vyombo vya habari ndivyo njia za kawaida za kueneza habari haraka kwa watu wengi.

Tumia mahali pa usambazaji kutekeleza shughuli mbali mbali kwa kutumia vipindi maarufu, kwa mfano michezo ya drama, vibonzo na hadithi simulizi n.k (zinazojumuisha burudani na ujumbe wa mawaidha au vyombo vya habari kupitia vipasa sauti, mabango, vijikaratasi, notisi, vibandiko, fulana n.k.

Ujumbe kupitia vyombo vya habari unaweza kusisitizwa na shughuli za ana kwa ana (mikutano). Shughuli hizi kwa mfano matembezi nyumbani zaweza kuwako kando na shughuli za usambazaji wa Vitu Visivyo Chakula yaani VVC.

Matembezi nyumbani hutoa nafasi kwa wakuza usafi kukadiri mandhari ya nyumbani na kuufanya ujumbe uwe wa kulenga mahitaji ya familia.

Vidokezo vya kutia maanani wakati wa matembezi nyumbani ni pamoja na:

- Matembezi yanafaa yafanywe kwa uangalifu. Hata wakati wa dharura, mienendo mingine inafaa kuangaliwa.
- Kwa kipimo mtoleaji mmoja anaweza kutembelea nyumba 5 – 6 (tano hadi sita) kwa siku moja ya kazi (masaa manne).
- Picha za maelezo kwa njia za chati za karatasi au kadi za picha ni muhimu sana kukuza ma zungumzo.
- Kupanga matembezi kunafaa kuwa kwa uangalifu na wana-kijiji wanahitaji kuelewa awali kabla ya matembezi. Katika hali za dharura watu watashughulikia vitu muhimu vya kujikimu kwa maisha.

> Mfuatilio

Kikao kimoja cha somo pekee **hakitoshi** kufunza njia na mbinu hizi. Masomo na mfuatilo yanafaa kufanywa baada ya masomo ya kwanza.

Wakuza usafi wanafaa kuweza kufuatila mabadiliko katika jamii kuhusu:

- Ridhisho???? wa watu kuhusu bidhaa iliyochaguliwa.
- Matumizi sawa za bidhaa
- Tabia za usafi wa matumizi na kuhifadhi maji kwa kila nyumba.

Je, chanzo cha maji kimechafuliwa?

Yes Ndiyo

La No Kuza kuhifadhna matumizi ya maji vyema

Je, bidhaa za kutoka nje ziko masokoni au zapatikana kutoka kwa mwito wa wafadhili?

LA No

Yes NDIYO

Je, maji ni machafu?

Je, maji ni machafu?

LA No

NDIYO Yes

Kuza chujio, kutumia vyungu vitatu, au kusafishakwa nguvu za jua na matumizi na kuhifadhi vyema mpaka ubora wa maji kuboreshwa au njia zingine kupatikana

NDIYO Yes

Kuza chujio, kutumia vyungu vitatu, mashapo kwa kemikali, au usafishaji wa kila mara kwa chujio. Pia kuza kuhifadhi na matumizi ya maji vyema.

LA No

Je, kuna moto ya kuni au njia nyingine ya moto?

Je, maji yana povu povu?

LA No

NDIYO Yes

Kuza chujio, kusafisha kwa nguvu za jua, kutumia vyungu vitatu au usafishaji wa kawaida kila mara kwa chujio. Pia kuza matumizi na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani.

Kuza chujio, kuchemsha na matumizi na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani. Pia kuza ukusanyaji usanyaji wa kuni kwa njia bora na kuhifadhi misitu upya

LA No


NDIYO Yes

Tumia donge ya kawaida ya kusafisha kwa kemikali. Pia kuza matumizi na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani.

Chuja maji na tumia donge mara mbili ya kusafisha kwa kemikali. Pia kuza matumizi na kuhifadhi vyema maji ya nyumbani.



Duniani kote, karibu bilioni moja ya watu hawana maji salama ya kwa kunywa. Watu bilioni 4, hasa watoto, hufa kila mwaka kwa sababu ya ukosefu wa maji salama.



Kwa miaka 15 iliyopita, Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu lime-shughulikia zaidi ya watu milioni 9 kwa mipango ya maji na usafi wa taka. Watu milioni 14 zaidi wanatarajiwa kufaidika kwa kifikia mwaka wa 2015.

> Vijikaratasi vya maelezo

Vijikaratasi hivi vifuatavyo vimekusudiwa kwa uchapishaji kwa wingi na kusambazwa kwa wanaohusika kwa mafunzo na usambazaji tofauti tofauti zilizoelzwa katika kitabu hiki cha mwongozo.

Kutumia vyungu vitatu

Kunywa maji: daima chota tu kutoka kwa mtungi wa tatu (3). Maji haya angalau yamehifadhiwa kwa siku mbili, na ubora wake umeongezeka. Baada ya muda wa siku kadhaa mtungi huu utasafishwa kwa maji moto sana.


a



b



c




Kutumia tiubu ya mpira au bomba la mpira kufanya maji kutoka kwa mtungi ni bora kwa sababu maji hayachafuki sana kama kutia.

Kila siku maji yanapoletwa nyumbani:

Kwa utaratibu tia maji yaliyo kwenye mtungi wa pili (2) kwenye mtungi wa tatu (3) Osha mtungi wa pili (2)

Kwa utaratibu tia maji yaliyo kwenye mtungi wa kwanza (1) kwenye mtungi wa pili (2) Osha mtungi wa kwanza (1)

Tia maji yaliyotekwa kutoka chanzo cha maji (ndoo nambari nne 4) kwenye mtungi wa kwanza (1) pitisha kwa chujio kukiwezekana.




Dokezo: Njia hii inaweza kuboreshwa kwa kutumia kitambaa cha kuchujia kila unapotia kwenye mitungi.


Jinsi ya kutibu maji kwa klorini ya maji ya WaterGuard (Sur'Eau)



Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.



Je, maji yako yanaonekana ni angavu?




Ongeza kifuniko kimoja kwa mtungi wa maji wa lita 20, kisha funikamtungi.



Je, maji yako yanaonekana ni chafu?




Chujia maji yako kwa kupitisha maji kwa kitambaa kisafi.




Ngoja kwa dakika thelathini.



Maji sasa ni tayari



Ongeza vifunikoviwili kwa mtungi wa maji wa lita 20, kisha funika mtungi.



Ngoja kwa dakika thelathini.




Maji sasa ni tayari

Jinsi ya kutibu maji kwa kutumia tembe za klorini



Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.



Je, maji yako yanaonekana ni angavu?




Ongeza kifuniko kimoja kwa mtungi kisha funika mtungi.



Je, maji yako yanaonekana ni chafu?




Chujia maji yako kwa kupitisha maji kwa kitambaa kisafi.




Ngoja kwa dakika thelathini.



Maji sasa ni tayari



Ongeza tembe mbili kwa mtungi kisha funika mtungi.



Ngoja kwa dakika thelathini.




Maji sasa ni tayari

Jinsi ya kutibu maji kwa kutumia Watermaker



1 Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.




2 Weka yaliyomo kwenye pakiti ya Watermaker katika ndoo.




5 Mimina maji yaliyotibiwa kwenye mtungi kwa kupitia kitambaa chujio.



6 Maji sasa ni tayari kwa kunywa




Koroga mchanganyiko yaliyomo kwa dakika tano



Ngoja kwa dakika kumi na tano



Usiyanywe maji yakiwa ni ya manjano.




Hifadhi maji kwenye mtungi mfasi na nuli ofunikwa

Jinsi ya kutibu maji kwa kutumia PUR



Nawa mikono yako kwa maji na sabuni au kwa jivu.



1. Kuchanganya

Weka yaliyomo kwenye pakiti ya PUR katika ndoo ya lita 10





3. Chujio

Tumia kitambaa kizito cha pamba kamili kisichokuwa na mashimo

Tupa chafu zilizochujwa mbali na watoto na wanyama


Mimina maji yaliyotibiwa kwenye mtungi kwa kupitia kitambaa chujio

2. Kukoroga



ikiwa maji si angavu baada ya dakika tano za kukongoja, koroga tena mpaka chafu zinazolowa kutengwa

Koroga mchanganyiko kwa dakika tano. Ngoja kwa dakika tano.



Ngoja kwa dakika ishirini.

4. Kunywa



Usiyanywe maji yakiwa ni ya manjano.

Maji sasa ni tayari kwa kunywa

> Habari zaidi

Vijikaratasi Vya Maelezo

<http://www.lboro.ac.uk/well/resources/fact-sheets/fact-sheets-htm/Household%20WT.htm>

Upimaji Ubora wa Maji Uwandani Katika Hali za Dharura

<http://www.lboro.ac.uk/well/resources/fact-sheets/fact-sheets-htm/WQ%20in%20emergencies.htm>

Kukuza Usafi

<http://www.ifrc.org/what/health/water/hygiene.asp>

Ubora Wa Maji Ya Kunywa

[http://www.who.int/water_sanitation_health/dwq/en/Maadili Kamili ya Kundi la Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu](http://www.who.int/water_sanitation_health/dwq/en/Maadili%20Kamili%20ya%20Kundi%20la%20Shirika%20la%20Msalaba%20Mwekundu%20na%20Hilali%20Nyekundu)

Maadili Kamili ya Kundi la Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

Wema na Utu

Kundi la Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu, lilianzishwa kunusuru waliojeruhiwa vitani, kwa shughuli zao za kila siku bila ubaguzi kwa uwezo wa kimataifa na nchini, kuzuia na kupunguza majuto kwa watu kila pahali. Lengo lake ni kutunza maisha na afya na kuhakikisha heshima kwa binadamu. Inakuza maelewano, urafiki, ushirikiano na amani ya kudumu kwa watu wote.

Kutopendelea upande wowote

Halibagui kwa sababu za uraia, kabila, imani za dini, cheo, au kisiasa. Inajaribu kupunguza majuto ya watu binafsi, kwa mwongozo wao na mahitaji yao, na kutoa usaidizi wa haraka kwa wanao dhiki.

Kutokuwa na upande

Ili kuwa wa watu wote, Kundi halitajishughulisha na upande wowote wakati wa uhasama au zogo lolote la kisiasa, la kikabila, kidini, na msimamo wa nadharia.

Uhuru

Kundi ni huru. Mashirika ya Kitaifa, ingawaje kwa kutoa huduma za fadhila kwa watu na serikali, kundi lazima lizingatii sheria za nchi zao na lazima kuwa huru ili kutekeleza majukumu yao kulingana na maadili ya Kundi.

Huduma ya kujitolea

Ni kundi la kujitolea kutoa fadhila na silo la kunuia faida yoyote.

Umoja

Msalaba Mwekundu mmoja au Hilali Nyekundu moja tu ndiyo itakuwa kwa kila nchi. Lazima kuwa wazi kwa wote. Kundi lazima litekeleze wadhifa wa fadhila nchini kote.

Kote duniani

Kundi la Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu, ambako mashirika yote yana usawa na kushirikiana kwa majukumu na kazi za kusaidiana liko kote duniani.



Kutunza Utu Wa **Binadamu** + C

Kutibu na kuhifadhi maji ya nyumbani

Kitabu hiki cha mwongozo kinanuiwa kwa wafanyi kazi na wajitolea wa Shirika la Msalaba Mwekundu / Hilali Nyekundu wanaoitikia dharura za shida ya maji. Kitabu hiki kinatoa nafasi kadha za kuboresha ubora wa maji.

Yaliyomo ni:

- Ubora wa maji kwa ufupi
- Jinsi ya kusafisha maji katika nyumbani kwa njia nyingi
- Jinsi ya kutumia maji ya nyumbani
- Jinsi ya kuchagua njia nzuri ya kuboresha maji nyumbani
- Jinsi ya kukuza kutibu na kuhifadhi maji ya nyumbani

Baada ya maamuzi na itikio, wafadhiliwa watahitaji mafunzo kamili ya kutibu maji. Kitabu hiki kina vijikaratasi vya maelezo vinavyoweza kusambazwa kwa matumizi na wajitolea kwa mafunzo.



Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu linakuza shughuli za kutoa huduma za fadhila kwa wanaoathirika na mashirika ya kitaifa.

Kwa kuratibu misaada kwa baa la kimataifa na kusisitiza muungano wa usaidizi unaotakikana kupunguza majuto ya binadamu.

Shirikisho la Kimataifa, Mashirika ya Kitaifa na Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu pamoja yanaunda Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na
Idara Ya Maji Na Usafu, Afya Na Utunzaji

Shirikisho la Kimataifa la Mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

S.L.P 372, CH-1211 Geneva 19, Switzerland

Telephone: +41 22 730 4222

Telefax: +41 22 733 0395

Barua pepe: secretarial@ifrc.org

Kwa maelezo zaidi, tazama mtandao wa shirikisho la kimataifa: www.ifrc.org